Maelezo juu ya dawa

An Dawa Za Kupigana Na Maambukizi Ya Vijidudu Vya Ukimwi

Dawa Za Kupigana Na Maambukizi Ya Vijidudu Vya Ukimwi

Dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi ni sehemu muhimu ya matibabu yako zidi ya maambukizi ya vijidudu vya ukimwi. Kwa kuwa vijidudu vya ukimwi ni vijimea vya aina yake tofauti vinavyoitwa “retrovirus”, dawa hizi kwa kawaida huitwa “**anti-retrovirals**”.

Kuna Aina Gani Za Dawa Za Kupigana Na Maambukizi Ya Vijidudu Vya Ukimwi?

Kuna aina/madaraja/makundi tofauti ya dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi. Aina mbalimbali za dawa hizi za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi hufanya kazi za kuzuia protini za aina mbalimbali ambazo vijidudu vya maambukizi ya ukimwi huitaji katika mfumo wao wa kuzaliana.

Kwa sasa, kuna aina kuu mbili za madaraja ya dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi zinazopatikana kwenye soko la madawa:

- Dawa ambazo zinazuia protini “**reverse transcriptase”,** inayojulikana kama **reverse transcriptase inhibitors** or **RT inhibitors (RTIs)**

Canadian AIDS Treatment Information Exchange
Réseau canadien d’info-traitements sida
www.catie.ca

AFRICANS IN PARTNERSHIP AGAINST AIDS
www.apaa.ca

Maamuzi juu ya matibabu ya aina mbalimbali yanahitajika kufanywa kwa kushauriana na mtaalamu aliyehitimu kwenye mambo ya afya na mwenye ujuzi juu ya magonjwa yanayoendana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi na matibabu atakayoamuliwa kutumiwa.

- Dawa ambazo huzuia protini "**protease**," inayojulikana kama **protease inhibitors (PIs)**

The RT Inhibitors (nukes and non-nukes)

RT inhibitors, au RTIs, zimegawanyika katika makundi matatu yanayoweza kutofautishwa kutokana na maumbile yao ya kikemia: **nucleoside RT inhibitors** (ambazo pia huitwa "**nukes**" or **NRTIs**) , **non-nucleoside RT inhibitors** (ambazo pia hiitwa "**non-nukes**" au "**NNRTIs**), na **nucleotide RT inhibitors** (ambazo pia huitwa **NtRTIs**).

Dawa kutoka katika daraja la **nukes** au **NRTIs** ni kama:

- AZT (ambayo pia hujulikana kama zidovudine au Retrovir)
- ddI (ambayo pia hujulikana kama didanosine au Videx au Videx EC)
- ddC (ambayo pia hujulikana kama zalcitabine au Hivid)
- d4T (ambayo pia hujulikana kama stavudine aur Zerit au Zerit XR)
- 3TC (ambayo pia hujulikana kama lamivudine au Epivir)
- abacavir (ambayo pia hujulikana kama ABC au Ziagen)
- Combivir (ambayo ni mchanganyiko wa dawa za AZT na 3TC)
- Trizivir (mchanganyiko wa dawa za AZT, 3TC na abacavir)

Dawa kutoka katika daraja la **non-nuke** au **NNRTI** ni kama:

- nevirapine (ambayo pia hujulikana kama Viramune)
- delavirdine (ambayo pia hujulikana kama Rescriptor)
- efavirenz (ambayo pia hujulikana kama Sustiva)

Dawa zilizokubalika kiviwango na kupitishwa kutoka daraja la NtRTU ni:

- tenofovir (ambayo pia hujulikana kama Viread)

The Protease Inhibitors (PIs)

Dawa za daraja la protease inhibitors ni kama:

- saquinavir (ambayo pia hujulikana kama Invirase na Fortovase)
- indinavir (ambayo pia hujulikana kama Crixivan)
- ritonavir (ambayo pia hujulikana kama Norvir)
- nelfinavir (ambayo pia hujulikana kama Viracept)
- amprenavir (ambayo pia hujulikana kama Agenerase)
- Kaletra (lopinavir na ritonavir)

Je, Muda Gani Unaweza kuwa Muafaka Kuanza Kutumia Dawa Za Kupigana Na Maambukizi Ya Vijidudu Vya Ukimwi?

Kuanza kutumia dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi ni uamuzi mkubwa. Unahitajika kuwa tayari kabla ya kuanza kutumia dawa hizi kwa kawaida zinahitajika kutumiwa muda uliopanga kutumia kila siku ili ziweze kufanya kazi vizuri.

Ni muhimu kutafuta daktari aliye na uelevu mzuri juu ya dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi, na ambaye atakuwa anaelewa hali yako na utamaduni wako atakapokuwa anakusaidia katika kufanya maamuzi yako juu ya matibabu haya.

Kwa kawaida, dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi zinashauriwa kuanza tumiwa kama:

- Kipimo chako ya chembechembe za T (zinazotumika kupima mfumo wako wa kupingana na magonjwa) ni chini ya 350.
- Ujazo wa vijidudu vya maambukizi ya ukimwi mwilini (unaotumika kupima ujazo wa vijidudu vya maambukizi ya ukimwi kwenye damu yako) ni zaidi ya 55,000.
- Kama umeshakuwa na dalili zozote za ugonjwa wa maambukiz ya vijidudu vya ukimwi.

Je, Dawa Gani Naweza kutumia?

Matibabu ya maambukizi ya vijidudu vya ukimwi kwa sasa hutumia mfumo wa matibabu unaotumia mchanganyiko wa walau dawa tatu za aina tofauti za dawa za

kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi kutoka kwenye madaraja mbalimbali.

Kuna sababu kuu 2 za kutumia mchanganyiko wa dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi kutoka madaraja mbalimbali kwa pamoja:

- Kutumia madaraja mbalimbali ya dawa hizi kutakuwezesha kuzuia aina mbalimbali za pritini ambazo vijidudu vya maambukizi ya ukimwi huhitaji katika hatua mbalimbali za kuzaliana, kwa hiyo tiba mchanganyiko hufanya kazi vizuri zaidi kuliko dawa kutoka kwenye daraja la aina moja tu.
- Vijidudu vya maambukizi ya ukimwi hubadilika kila vinapojizaa upya na huweza kuwa sugu na aina moja ya dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi, na kumaanisha kuwa dawa hizo hazitafanya kazi ya kupigana na vijidudu hivyo tena. Kama dawa za aina mbalimbali zinatumika kwa pamoja, ni vigumu kwa vijidudu kujibadilisha na kuweza kuwa sugu kwa dawa zote kwa wakati mmoja
- Wakati wa kuchaguwa dawa gani zitumike kwenye mchanganyiko wako, daktari wako anahitajika kufanya uamuzi huu pamoja na nawe akizingatia mchanganyiko ambao:
- unachanganya aina tofauti za dawa za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi (ambazo zitashambulia vijidudu vya maambukizi ya ukimwi katika hatua zake mbalimbali za kuzaliana)
- utakuzidishia uwezo wako wa kutumia dawa mara kwa mara.
- utapunguza madhara yatokanayo na matumizi ya dawa mbalimbali
- utakuwezesha kubadilisha dawa huko mbeleni kama itahitajika.

Muulize daktari wako au mfamasia wako juu ya maelezo zaidi ya dawa zilizopendekezwa kwa matumizi yako, na waeleze juu ya mambo yote unayowaza kabla ya kuanza kuzitumia.

Je, Nitajuwaje Kama Dawa Zangu Zinafanya Kazi Vizuri?

Kama dawa zako za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi zinafanya kazi

vizuri (yaani kama zinafanya kazi vizuri ya kutawala na kupigana na vijidudu vya maambukizi ya ukimwi), utatakiwa kutegemea:

- kupungua kwa ujazo wa vijidudu vya maambukizi ya ukimwi mwilini (walau hadi kwenye kiwango cha “kutoweza tambulika”)
- Ongezeko la katika kipimo chako cha chembechembe za T.
- Kupungua kwa maambukizi na dalili mbalimbali zinazoendana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi.
- Afya nzuri kwa ujumla.

Kwa kwenda kwa daktari wako mara kwa mara ka ajili ya kutazama afya yako na kufanya vipimo kadhaa vya damu kuweza juwa juu ya ujazo wa vijidudu vya maambukizi ya ukimwi mwilini na kipimo chako cha chembechembe za T, kunaweza kukusaidia kuelewa na kuona kama dawa zako zinafanya kazi vizuri mwilini mwako.

Je, Ni Wakati Gani Nahitajika Kubadilisha Dawa Zangu?

Unahitajika kubadilisha dawa zako za kupigana na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi katika mchanganyiko wako kama:

- Dawa unazotumia hazifanyi kazi yake vizuri (hali hii huitwa “kushindwa kwa matibabu”)
- Dawa unazotumia zinakupatia madhara mabaya baada ya kuzitumia

Kama unahitaji kubadilisha dawa zako kwa kuwa mchanganyiko wako haufanyi kazi vizuri, yaani hauwezi kupigana na vijidudu vya maambukizi, daktati wako atahitajika kubadilisha walau aina 2 kati wa 3 ya dawa zilizopo kwenye mchanganyiko wako, au wakati mwingine zote 3. Kama utakuwa umeshatumia dawa nyingi za aina mbalimbali za kupigana na maambukizi ya ukimwi, daktari wako anahitajika kukufanyia kipimo maalumu, kinachoitwa “kipimo cha usugu” au “resistance testing,” kabla ya kukubadilishia dawa. Kipimo hiki kitawasaidia wewe na daktari wako kutambua dawa gani hazitafanya kazi zidi ya maambukizi ya vijidudu vya ukimwi mwilini mwako.

Kama unapatwa na madhara mabaya baada ya kutumia dawa zako, daktari wako anaweza kukushauri kupunguza kiwango unachomeza cha dawa ambayo inakusababishia matatizo au kubadilisha dawa hiyo na kukupatia nyingine. Kwa mantiki hii, hutahitajika kubadilisha dawa zako kwa kuwa zinafanya kazi vizuri.

Jinsi tunavyozidi kujifunza zaidi juu ya madhara ya dawa za kupigana na maambukizi ya ukimwi na jinsi dawa mpya zinavyogunduliwa, maelekezo ya jinsi gani matibabu yanaweza fanyika yataweza badilika pia. Tafadhali hakikisha unashirikiana na kufanya kazi pamoja na daktari wako na mfamasia wako kuweza kujuwa maelezo ya karibuni juu ya matibabu mbalimbali na kuweza kuchaguwa mchanganyiko gani wa dawa utaweza kukutibu vizuri kutokana na mahitaji yako.

Shirika la kubadilishana maelezo juu matibabu ya ukimwi Kanada (The Canadian AIDS Treatment Information Exchange – CATIE) na Shirikisho la waafrika katika kupigana na ukimwi (Africans in Partnership Against AIDS - APAA) kwa nia nzuri kabisa wanatoa maelezo kwa watu wanaoishi na maambukizi ya vijidudu vya ukimwi/Ukimwi ambao wangependa kutawala afya zao wenyewe kwa kushirikiana na wataalamu wa afya wanaowapatia matibabu. Hata hivyo, maelezo haya yanayochapishwa au kutolewa na CATIE au APAA hayawezi kuchukuliwa kama ushauri wa kiafya. Hatushauri au kusisitiza juu ya tiba moja juu ya nyingine. Hivyo tunawashauri watumiaji ya maelezo yetu kupitia maelezo ya matibabu mengine yanayotolewa na vyanzo mbalimbali kwa upeo mkubwa iwezekanavyo. Tunawashauri watumiaji wa maelezo haya na kusisitiza kuwa ni muhimu kushauriana na wataalamu ya afya na tiba waliohitimu mafunzo yao kabla ya kuamua, kutumia au kuanza jambo lolote juu ya matibabu.

Vile vile, hatuthibitishi au kudhamini ukweli au ufarisi na ujuzi wa maelezo yanayochapishwa au kupatikana kutoka CATIE au APAA. Watumiaji wanaotumia au kutegemea maelezo haya wanafanya hivyo kwa kuthubutu wenyewe na matokeo yake yakiwa mabaya yatakuwa juu yao. Si CATIE wala APAA, au Wizara ya Afya Kanada, au wafanyakazi wao, wakurugenzi, maafisa au watu wanaojitolea wataweza kuhusishwa na uharibifu wa aina yeyote unaoweza kutokea kwa kutumia vizuri au vibaya maelezo haya. Mawazo na maelezo yaliyotolewa hapa au kwenye nakala yeyote au ilani/tangazo lolote.

Copyright: This Fact Sheet is made available through a collaboration between Africans in Partnership Against AIDS (APAA), Asian Community AIDS Services (ACAS) and the Canadian AIDS Treatment Information Exchange (CATIE). Original content developed by ACAS, 2001. Translation into Swahili and Hausa by APAA, 2004.

This information is also available in Chinese, Tagalog and Vietnamese

Funding has been provided by Health Canada, under the Canadian Strategy on HIV/AIDS

Supported by an unrestricted educational grant from GlaxoSmithKline in partnership with Shire BioChem

ACAS Asian Community AIDS Services
www.acas.org

Canadian Strategy on HIV/AIDS

GlaxoSmithKline

Shire BioChem